# Utafiti wa Lugha ya Nyumbani ya Georgia

**Mwanafunzi :** ______________________________________ **Mwalimu :** _______________________________________

**Ilani kwa Wazazi na Walezi:**
Mifumo ya shule ya Georgia inahitajika[1] ili kukusanya majibu yako[2] kwa maswali kuhusu lugha unayopendelea kwa mawasiliano ya shule na lugha ya msingi au ya nyumbani ya mtoto wako. Taarifa kutoka kwa swali la kwanza hutumiwa kutambua hitaji lako la mkalimani au hati zilizotafsiriwa. Taarifa kutoka kwa maswali matatu *ya Utafiti wa Lugha ya Nyumbani* na maelezo ya ziada ya lugha hutusaidia kubainisha iwapo tutachunguza kiwango cha mtoto wako cha ustadi wa lugha ya Kiingereza. Mchakato wa kukagua utabainisha iwapo mtoto wako anahitimu kwa kiwango cha kuwa mwanafunzi wa Kiingereza na huduma katika mpango wetu wa elimu wa mafundisho ya lugha.

| Madhumuni ya Maswali | Maswali & Majibu ya Mzazi/Mlezi |
|---|---|
| **Mapendeleo ya Mawasiliano**<br><br>Swali hili husaidia shule kukupea mkalimani au hati zilizotafsiriwa, bila malipo, iwapo unahitaji.<br><br>Swali hili ni kwa madhumuni ya habari tu . **Halitumiwi** kuchunguzi umahiri wa mtoto wako kwenye lugha ya Kiingereza. | **Lugha ya Mawasiliano ya Mzazi (Inahitajika)**<br><br>• Je, ungependa kupokea mawasiliano ya shule katika lugha gani?<br>_________________________________ |

| | |
|---|---|
| **Utambulisho wa Wanafunzi Wanaoweza Kujifunza Kiingereza**<br><br>Maswali haya matatu husaidia shule kutambua ikiwa mtoto wako anafaa kuchunguzwa ili kubaini kustahiki kwake kushiriki katika mpango wake wa elimu ya lugha.<br><br>Wakati jibu la swali lolote kati ya haya ni lugha nyingine isipokuwa Kiingereza, shule zinaweza kuhitajika kuchunguza kiwango cha mtoto wako cha ujuzi wa lugha ya Kiingereza. Ukijibu na zaidi ya lugha moja, shule itahitaji maelezo ya ziada kutoka kwako kabla ya kufanya uamuzi huu. | **Utafiti wa Lugha ya Nyumbani (Inahitajika)**<br><br>1. Je, mtoto wako anaelewa na kuzungumza lugha gani vizuri zaidi? __________<br>2. Mtoto wako huzungumza lugha gani mara nyingi akiwa nyumbani? ___________<br>3. Ni lugha gani ambayo watu wazima nyumbani kwako hutumia mara nyingi wanapozungumza na mtoto wako?<br>___________________________ |

| | |
|---|---|
| **Maelezo ya Ziada kutoka kwa Familia zinazotumia Lugha nyingi**<br><br>Iwapo uliashiria kuwa mtoto wako na watu wazima wengine nyumbani ***wanaelewa na kutumia Kiingereza na lugha nyingine*** au zingine, shule zitakuomba utoe maelezo ya ziada ili kutadhmini iwapo mtoto wako anapaswa kuchunguzwa ujuzi wa Kiingereza.<br><br>Ukijibu kwamba mtoto wako anaelewa na kutumia Kiingereza zaidi kuliko lugha nyingine ya nyumbani au kwamba mtoto wako anaelewa na kutumia Kiingereza na lugha nyingine ya nyumbani kwa usawa, shule haitamkagua mtoto wako ujuzi wa lugha ya Kiingereza. | **Maelezo ya Ziada kutoka kwa Familia zinazotumia Lugha nyingi.** ***Chagua sentensi moja pekee inayofafanua vyema lugha ya msingi ya mtoto wako.***<br><br>☐ Mtoto wangu anaelewa na anatumia lugha ya nyumbani pekee na **si Kiingereza**.<br>☐ Mtoto wangu anaelewa na anatumia zaidi lugha ya nyumbani na **Kiingereza kidogo**.<br>☐ Mtoto wangu anaelewa na anatumia lugha ya nyumbani na Kiingereza **kwa usawa.**<br>☐ Mtoto wangu anaelewa na anatumia **zaidi Kiingereza** na kidogo tu ya lugha ya nyumbani.<br>☐ Mtoto wangu anaelewa na anatumia **Kiingereza pekee**. |

**Sahihi ya mzazi :** _______________________________________ **Tarehe:** _________________________________

[1] U.S. Department of Justice, Civil Rights Division, and U.S. Department of Education, Office for Civil Rights, 7 January 2015, *Dear Colleague Letter: English Learner Students and Limited English Proficient Parents, p. 10.*
[2] Utafiti wa Lugha ya Nyumbani unapaswa kutolewa kwa waliojiandikisha kwa mara ya kwanza katika shule za umma za Marekani.